# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## VETA

CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA VETA TABORA

MKATABA WA FUNDI UJENZI

**1.0 Maelezo ya mkataba**

i) Jina la mkataba: - KAZI YA KUTENGENEZA NA KUFUNGA MADIRISHA YA ALUMINIUM KWA MAJENGO KUMI NA MOJA.

ii) Na. ya mkataba: VETA/TBR/UYUI/DVTC/PHASE II/02

**2.0 Makubaliano:**

Makubaliano haya yamefanyika leo siku ya Ijumaa.......................Tarehe 24/06/2022 mwezi 06........................ Mwaka 2022......................... Kati ya Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma VETA Tabora (Tabora RVTSC) wa S. L. P. 2060........................ Tabora, ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 Dodoma (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

TAWAQAL SEIF SAMBIRO wa S. L. P. 11001, Mwanza (ambaye hapa anatambulika kama Fundi).

Kwamba mwajiri anampatia Fundi kazi ya kutengeneza, kuleta na kufunga madirisha ya alluminium katika chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya Uyui (Uyui DVTC) ambacho kinaendelea na ujenzi kama ifuatavyo:-

Alluminium Sliding Windows

i) Computer Class Size: 2800 X 1800mm High 14 Pcs Tsh10,640,000.00

ii) MVM na WF Karakana 3770 X 1800mm high 9 Pcs Tsh 8,820,000.00

iii) Maliwato (Vyoo) (a) 1000 X 600mm High 18 Pcs Tsh 3,600,000.00

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (b) 2000 X 600mm high 6 Pcs | Tsh 1,740,000.00 |
| iv) | Jengo la Stoo | (a) 1600 X 1800mm high 1 Pc | Tsh 620,000.00 |
| | | (b) 800 X 750mm high 2 Pcs | Tsh 170,000.00 |
| v) | Aluminiu partition: White with 6mm half clear glass (upper part) and 5mm half frosted (bottom part) also MDF board cherry with two (2) Doors of size 900 X 2100mm and Talking hole of 6750mm X 3200mm and 3000mm X 3200mm | | Tsh 3,200,000.00 |

**Jumla**

**Tsh 28,960,000.00**

Kwamba kazi hizi zitafanyika katika eneo la chuo cha Ufundi cha Wilaya ya Uyui lililopo eneo la Idete mkabala na shule ya sekondari ya Idete, Wilaya ya Uyui katika mkoa wa Tabora.

Gharama ya kazi hizi zote ni jumla ya **Shilingi 28,960,000.00.** Kwa **maneno, (Shilingi Milioni Ishirini na nane laki tisa elfu sitini tu).**

Kwamba kazi hizi zitachukua muda wa siku..30.. kwa maneno (...Therathini...) mpaka kukamilika.

## 3.0 Awamu za Malipo:

Malipo itakuwa kama ifuatavyo:

- Awamu ya kwanza Advance Payment ni Tsh 14,480,000.00 Shilingi Milioni Kumi nan ne laki nne elfu themanini tu)

- Awamu ya pili ya malipo baada ya kumaliza ni Tsh 14,480,000.00 (Shilingi Milioni Kumi nan ne laki nne elfu themanini tu)

**4.0 Mwajiri:**

Kwamba mwajiri amekubali gharama zilizotolewa na Fundi kwa kazi zilizotajwa hapo juu.

**5.0 Fundi:**

Fundi amekubali kuzifanya kazi hizo za kutengeneza, kuleta na kufunga madirisha ya alluminium kwa kusimamiwa na Msimamizi wa ujenzi pamoja na kamati ya ujenzi kwa gharama zilizoelezwa hapo juu na kuikamilisha kwa siku zilizotajwa hapo juu.

**6.0 Mwajiri na Fundi kwa pamoja wamekubaliana:**

i Kwamba kazi zitafanyika kwa kiwango cha hali ya juu kwa mujibu wa viwango vya majengo ya serikali na kama vipimo katika BoQ vinavyosema.

ii Kwamba kabla ya malipo kazi zitakaguliwa na Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui aliyeteuliwa kukagua kazi za ujenzi wa chuo cha ufundi Uyui.

iii Kwamba Fundi hataendelea na hatua nyingine ya ujenzi mpaka hatua ya awali imekaguliwa na kukubalika na Mhandisi wa Wilaya na kamati ya ujenzi.

iv Kwamba iwapo itabainika kwamba Fundi amejenga kinyume na maelekezo ya Msimamizi wa ujenzi, Fundi atawajibika kubomoa na kurekebisha kwa gharama zake.

vi Kwamba malipo yatalipwa pale tu ambapo awamu husika ya ujenzi imekamilika na imekaguliwa na Mhandisi wa Wilaya ya Uyui pamoja na kamati ya ujenzi na kuthibitishwa kwa maandishi.

vii Kwamba malipo yote yatalipwa kupitia mfumo wa malipo serikalini (MUSE) kwa hiyo Fundi anatakiwa kuwa na akaunti benki.

viii Kwamba endapo itabainika kuwa Fundi anakiuka mashariti ya mkataba huu bila sababu za msingi, uongozi wa chuo cha ufundi VETA Tabora utafuta/utavunja mkataba huu na Fundi hatalipwa chochote na hatua za kisheria zitachukuliwa.

**7.0 Kodi ya zuio (Withholding Tax)**

Malipo yote yatakatwa kodi ya zuio ya asilimia tano (Withholding Tax 5%) kama sheria za kodi zinavyosema.

**8.0 Fedha ya zuio (retention fund)**

Mwishoni mwa kazi iliyoanishwa katika Mkataba huu, Mwajiri atabaki na 5% ya gharama ya ujenzi hadi pale muda wa matazamio ya ujenzi (miezi sita) utakapokwisha. Fedha hizo zinaweza kutumika pale tu ambapo kuna uharibifu umetokea katika ujenzi ndani ya kipindi cha matazamio ya ujenzi na Fundi akashindwa au akakataa kurekebisha uharibifu huo ndani ya muda wa majuma mawili (2) baada ya kupata maelekezo ya Mwajiri.

**9.0 Nyaraka zinazokamilisha mkataba huu ni:**

- Hati za bei za Fundi
- Michoro na vipimo vya majengo
- Barua ya kukubali kazi ya Fundi
- Mkataba wenyewe

**10.0 Saini za pande zote mbili:**

Imetiwa saini na

**MWAJIRI**
Jina: Dkt. Kyomo, Z. B. ........
Cheo: Mkuu wa Chuo
Saini: ..............................

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UFUNI JA HUDUMA
TABORA

**SHAHIDI**
Jina: Raphary B. Mdambete
Cheo: EGRAO
Saini: ..............................

**FUNDI**
Jina: Tawaqal Sambiro
Saini: ..............................

TAWAQAL SEIF SAMBIRO
S.L.P 11001
MWANZA
TIN: 114-777-803

**SHAHIDI**
Jina: Ayoub Shaban
Saini: ..............................